

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

NAMBA ZA SIMU: 0786871008
0737800229

SHULE YA SEKONDARI CHIKONJI,
S.L.P 717,
LINDI.

06/12/2020

MWANAFUNZI

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA I MWAKA 2021 SHULE YA SEKONDARI CHIKONJI

1.0 Ninapenda kukutarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari chikonji kwa mwaka wa masomo 2021. Shule ya sekondari chikonji ipo manispaa ya lindi katika mkoa wa LINDI. Muhula wa kuanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti bila kuchelewa shule tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 29/01/2021. Baada ya tarehe hiyo msako wa wanafunzi ambao hawajaripoti utafanyika na mzazi ambaye hatamleta mtoto wake shuleni atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni kulipa faini au kifungo au vyote kwa pamoja.

2.0 SARE ZA SHULE

a) Sare za shule hii ni

WAVULANA

- Suruali ndefu mbili za rangi ya (kharoti) mshomo unaokubalika, si kubana (Modal) wala si pana sana (Bagi) kitambaa kizito.
- Shati mbili nyeupe (Tetron) mikono mifupi.
- Mkanda wa ngozi mweusi bacos ya kawaida kwa wavulana.
- Viatu vyeusi vya kamba (Gidam) vya ngozi vyenye kisigino na shingo fupi.
- Jozi mbili za soksi nyeupe kwa wote.

WASICHANA

- Sketi mbili za rangi ya kharoti kitambaa kizito, urefu kupita magoti mshono wa rinda boksi.
- Shati nyeupe (Tetron) 2 mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya Kamba (Gidam) vya ngozi vyenye kisigino kifupi na shingo fupi (**Vibajaji marufuku kabisa**).
- Jozi mbili za soksi nyeupe kwa wote.

b) Kwa wale wanaovaa **HIJABU** inatakiwa iwe nyeupe ndefu na sio kibwaya wala isiyo bana (**kitambaa kizito sio mpira**) pia ivaliwe na **nusukanzu** (**kitambaa kizito sio mpira**) na sketi ndefu.

- ❖ Madaftari yasiyopungua 15 makubwa (counter book)
- ❖ Kalamu za kutosha
- ❖ Mathematical set
- ❖ Dictionary (**kwa matumizi ya kujifunzia kingereza**)
- ❖ Rimu moja A4 kwa ajili ya mitihani
- ❖ Faili moja kwa ajili ya kutunzia mitihani yake, ni vizuri zaidi mwanafunzi akanunuliwa boxfile kwani atatumia mitihani mingi zaidi na kwa usalama.

c) **SARE ZA MICHEZO:-**

1. **WAVULANA**

- BUKTA, TISHETI NA SOKSI ZA MPIRA RANGI YA BLUE
- RABA ZA MICHEZO

2. **WASICHANA**

- TRACK NA TISHETI RANGI YA BLUE
- RABA ZA MICHEZO

3.0 VIFAA VYA USAFI (AJE NAVYO MWANAFUNZI SIKU YA KUJA KURIPOTI)

i. **WASICHANA** - Ndoo ndogo mpya yenye mfuniko.

ii. **WAVULANA** - Ndoo ndogo mpya yenye mfuniko.

4.0 KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE KWA MUJIBU WA SHERIA NCHINI

Shule ya sekondari CHIKONJI ni shule ya serikali inayoendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25 ya mwaka 1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayototewa na wizara yenye dhamana ya Elimu Nchini. Ukiwa mwanafunzi katika shule hii unatakiwa kuzingatia na kuheshimu mambo ya msingi yafuatayo, ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- A. Kila mwanafunzi anawajibika kuwa naheshima na adabu kuanzia nyumbani, shuleni na mitaani.
- B. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya, kati yake na mwanafunzi mwenzake, kwa walimu na watu wengine wanaomzidi umri.
- C. Ni lazima kuonesha moyo wa kushirikiana, huruma, upole na kusaidiana katika shughuli mbalimbali pamoja na kazi.
- D. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kusalimia na kupokea mzigo wa mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri.
- E. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba za walimu bila idhini toka kwa Mkuu wa shule.
- F. Wanafunzi hawaruhusiwi kufanya mambo yafuatayo.
 - i. Kuvuta sigara/bangi.
 - ii. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama kulegeza suruali na nguo za kubana.
 - iii. Kutumia madawa ya kulevya.
 - iv. Kupiga kelele darasani
 - v. Kufuga kucha ndefu, kuwa na nywele zisizokubalika na chafu, kuwa mapambo, kujipaka rangi katika kucha na midomo (hasa wasichana)
 - vi. Kunyoa nywele katika mitindo isiyokubalika.
 - vii. Kuchelewa kufika shule kwa makusudi, kutofanya kazi katika eneo alilopangiwa na kutohudhuria vipindi darasani.
 - viii. Kutochomea shati na kuvaa suruali bila mkanda (wavulana).
 - ix. Ni marufuku kuvaa viatu vya wazi (sandals).

- x. Ni wajibu wa mzazi kutoa taarifa endapo mwanafunzi amepata matatizo ya kiafya au kifamilia.
- xi. Wanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka wakiwa shuleni, wala kufuga nywele ndefu.
- xii. Kuingia kumbi za starehe, kwenda kwenye vigodoro, kuangalia video kwenye kumbi za video, vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni.

G. Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa shule kwa mwanafunzi.

- i. Wizi,
- ii. Uasherati, ubakaji na ushoga, ulawiti na usagaji.
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yoyote ya kulevya.
- iv. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake au mtumishi au mtu mwingine yeyote Yule ndani au nje ya shule.
- v. Makosa ya jinai (kuua, kuiba)
- vi. Kuharibu kwa maksudi mali ya shule / umma (ya watu wengine.)
- vii. Kuoia au kuolewa, kupata **mimba** au kusababisha **mimba** ndani na nje ya shule.
- viii. Kutoa **mimba** au kushawishi kutoa **mimba**.
- ix. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kuvuruga Amani na usalama wa watu.
- x. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xi. Kutohudhuria shule bila taarifa (**Utoro**)
- xii. Kudharau bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Taifa, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.
- xiii. Kujiachisha shule mwenyewe.
- xiv. Kutumia au kumiliki simu.

H. Ni kosa kutoelewa sheria za shule kwa mwanafunzi na watumishi wote wa shule.

“KARIBUNI SANA CHIKONJI SEKONDARI”

.....
RAMADHAN YUSSUF AHMAD
MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

SHULE YA SEKONDARI CHIKONJI,
S.L.P 717,
LINDI.
TAREHE

KUMB. NA. CHSS/FI/MED.EXAM/2021

.....

MGANGA MFAWIDHI

YAH: MWANAFUNZI

Amechaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya sekondari CHIKONJI mwezi Januari 2021. Kiutaratibu kabla ya kukubaliwa kuingia katika shule hii kuendelea na masomo ni lazima apimwe afya kwanza, ili itusaidie kutambua afya yake akiwa shuleni.

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika hapa nchini baada ya kupimwa.

Ahsante kwa ushirikiano

.....
RAMADHAN YUSSUPH AHMAD
MKUU WA SHULE

Tafadhali oneshwa kama mwanafunzi mhusika amewahi au ana magonjwa yafuatayo kwa kuweka alama (✓) sehemu inayohusika.

- | | | |
|--|------------|--------------|
| 1. Kifafa (Epilepsy) | Ndio | Hapana |
| 2. Moyo (Hearth Disease) | Ndio | Hapana |
| 3. Magonjwa ya akili (Mental case) | Ndio | Hapana |
| 4. Ukosefu wa damu (Anemia siclecell) | Ndio | Hapana |
| 5. Kifua kikuu (T.B) | Ndio | Hapana |
| 6. Pumu (Asthmatic case) | Ndio | Hapana |
| 7. Kisukari | Ndio | Hapana |
| 8. Kichocho (Bilharzias) | Ndio | Hapana |
| 9. Malaria sugu (Chronic Malaria) | Ndio | Hapana |
| 10. Magonjwa ya zinaa (Vernadal disease) | | |
| 11. Ujauzito | Ndio | Hapana |
| 12. Je? Ana dosari nyingine yoyote ile ya kiafya | Ndio | Hapana |

KAMA NDIO TOA
MAELEZO.....
.....
.....

JINA LA MGANGA MFAWIDHI:

SAHIHI:

TAREHE:MHURI WA OFISINI.....

TAARIFA MAALUMU YA KUHUSU MWANAFUNZI

SEHEMU "A" (HERUFI KUBWA)

Jina kamili

Tarehe ya kuzaliwa

Anwani ya nyumbani

Kata Jina la mtendaji katano ya simu.....

Mtaa Jina la mtendaji wa mtaano ya simu.....

SEHEMU "B"

Jina la baba mzazi/mlezi

Kazi ya baba mzazi/mlezi..... Namba ya simu

Jina la Mama mzazi/mlezi.....

Kazi ya Mama mzazi/mlezi Namba ya simu

SEHEMU "C"

Taarifa za ndugu wa karibu

JINA LA NDUGU	UHUSIANO	KIWANGO CHA ELIMU	ANWANI/NAMBA YA SIMU

SEHEMU D

Michezo/Sanaa anayoipenda

JINA LA MCHEZO	SHULE	TOKA MWAKA	HADI MWAKA

SEHEMEMU E

Kazi yoyote/ uongozi aliowahi kufanya

KAZI/CHEO	SHULE	TOKAMWAKA	HADI MWAKA

1. Ninaahidi kuwa na tabia nzuri mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.
2. Nitafuata taratibu na sheria nitakazoelekezwa nitakapoenda kinyume na sheria ichukuwe mkondo wake.
3. **UTORO KWANGU NI MWIKO.**

Sahihi ya Mwanafunzi

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

Tarehe

AHADI YA MZAZI KUKUBALI MWANAE KUJIUNGA NA SHULE

Mimi:.....Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi..... Ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari CHIKONJI, kidato cha kwanza mwaka 2021.

- i. Ninakubali/sikubali mwanangu asome katika shule hii.
- ii. Ninaahidi nitatii/ sitatii na kumuhimiza mwanangu kutii/ kutotii sheria zote kwa mujibu wa kanuni na taratibu kama nilivyofahamishwa na uongozi wa shule.
- iii. Nakubali/sikubali mwanangu kuadhibiwa kwa mujibu wa taratibu endapo atavunja au kukiuka sheria za shule.
- iv. Wakati wote mwanangu atakapokuwa shuleni (Mwanafunzi) hana ruhusa ya kwenda kwenye nyumba za wageni, maeneo ya ulevi, kumbi za sinema,kucheza pool table,kamari kwenda kwenye Vigodoro na muziki.
- v. Ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika kwa wakati.
- vi. Ninaahidi kumleta shuleni kwa wakati bila kumchelewesha.
- vii. Ninaahidi kushirikiana na walimu katika kufuatilia maendeleo ya mtoto (Kitaaluma,Kinidhamu n.k)
- viii. Ninaahidi nitahudhuria vikao vyote pindi nitakapohitajika.

KUKUBALI SHERIA ZA SHULE

A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

Jina la Mwanafunzi:

Tarehe ya kuzaliwa:

Uhusiano (Undugu na mlezi, baba, mjomba, kaka n.k):

Mimi

- Nikiwa mwanafunzi wa shule hii nakubali kuwa Umma wa Nchi ya Tanzania ndio ulionipa nafasi hii maalum ya masomo, ili nimalizapo niweze kutumikia Nchi katika maendeleo yake.
- Hivyo naahidi kwamba nitajibidiisha hapa shuleni na pia nimalizapo shule ili kutimiza shabaha hiyo, ninakubali na kuahidi kwa hiyari yangu mwenyewe na nitatii sheria za shule na amri zote nitakazopewa iwapo nitakiuka sheria za shule.

B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi

Ambaye ni Mzazi /Mlezi wa mwanafunzi tajwa hapo juu, naahidi kutoa ushirikiano mzuri na uongozi wa shule katika kumlea mwanangu.

Nitakuwa tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala la nidhamu ya mwanafunzi na kwamba niko tayari kukubaliana na adhabu itakayotolewa iwapo mwanafunzi atakuwa amehusika na utovu wa nidhamu.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI:

TAREHE:

**OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI
“SHULE YA SEKONDARI CHIKONJI”**

MKATABA WA MAKUBALIANO BAINA YA MZAZI, MWANAFUNZI NA SHULE YA SEKONDARI CHIKONJI

1. Shule ya sekondari CHIKONJI kama zilivyokuwa shule nyingine zote zilizosajiliwa kisheria kutoa huduma katika jamii chini ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina taratibu na sheria zinazotumika katika kuiongoza shule.

Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais John Magufuli kupitia waraka namba 5 wa **ELIMU MSINGI BILA MALIPO** umekusudia kuhakikisha wanafunzi wote wanasoma bila vikwazo na wazazi na jamii kwa jumla kuwasimamia katika usomaji wao.

Kupitia waraka huo shule ya sekondari CHIKONJI itatekeleza majukumu yake yote yaliyoagizwa na serikali ya kumfundisha na kumuandaa Mwanafunzi ili kuweza kufaulu na kutopata sifuri “Division zero” katika mitihani ya kidato cha pili na cha nne.

RAMADHAN YUSSUPH AHMAD
MKUU WA SHULE

Saini

2. TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi _____ Mwanafunzi wa kidato cha 2021 hapa shule ya sekondari CHIKONJI ninafundishwa na kuandaliwa kufanya mtihani wa kidato cha pili na nne.

Ninakiri kuwa ninafundishwa na kuandaliwa ili **KUTOPATA SIFURI “DIVISION ZERO”**. Nikifeli Mitihani hiyo kwa kupata **DIVISION ZERO** itakuwa ni uvivu na uzembe wangu mimi kwa kuwa nimefika kidato cha kwanza/tatu kwa kuwa nina sifa na uwezo wa kusoma kwa sababu nilifaulu mtihani wa darasa la saba kutokana na juhudi na uwezo wangu wa kusoma. Na nikifeli niwajibishwe.

Saini ya Mwanafunzi

Tarehe

3. TAMKO LA WAZAZI

Mimi _____ Mzazi/Mlezi wa _____ Mwanafunzi wa kidato cha wa shule ya sekondari chikinji. Ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa waraka wa serikali namba 5 wa **ELIMU MSINGI BILA MALIPO** na majukumu yangu yaliyoagizwa na serikali katika waraka huo nitayatekeleza ili kuhakikisha mwanafunzi anafaulu mitihani yake na **KUTOPATA SIFURI “DIVISION ZERO” KATIKA MITIHANI YAKE**. Endapo atafeli kwa kupata **SIFURI “DIVISION ZERO”**. Na ikiwa kufeli kumesababishwa na mimi Mzazi/Mlezi kushindwa kutekeleza majukumu yangu nitakuwa tayari kuwajibika kutokana na sheria za Nchi zilivyo na nitajieleza katika baraza la kata.

Saini ya Mzazi

Tarehe

4. OFISI YA SERIKALI YA KATA

Saini ya Mtendaji wa Kata

Tarehe

Muhuri